

# PBPA



Toleo Na. 05 | Juni, 2026

# Bulletin



# Kamati ya Uhariri

---

Lilian Rwegimbura

MWENYEKITI

Sarah Mwakyusa

KATIBU

Matiko Sanawa

MJUMBE

Henry Kilenga

MJUMBE

Rehema Mahundi

MJUMBE

Nyamhoni Chacha

MSANIFU

# Yaliyomo

|                                                                                                   |    |
|---------------------------------------------------------------------------------------------------|----|
| Tanzania Yaendelea Kuwa Kitovu Cha Mafunzo na Usafirishaji wa Mafuta Kanda ya Afrika              | 03 |
| PBPA Yaagizwa Kuongeza Kasi ya Upokeaji na Usambazaji wa Mafuta Nchini                            | 06 |
| NDEJEMBI: Serikali Yahakikisha Upatikanaji wa Mafuta Licha ya Vita Inayoendelea Mashariki ya Kati | 08 |
| Teknolojia ya SCADA Ilivyosaidia Kupunguza Upotevu wa Mafuta Nchini                               | 11 |
| Baraza la Wafanyakazi PBPA Lahimizwa Kuwa na Uadilifu Katika Kuwakilisha Maslahi ya Watumishi     | 14 |
| Watumishi PBPA Wahamasishwa Kupima Afya na Kupata Chanjo ya Homa ya Ini                           | 17 |
| PBPA Yahitimisha Kwa Mafanikio Ushiriki Wake Katika Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma 2026  | 20 |
| PBPA Yahamasisha Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia                                              | 23 |



# Tanzania Yaendelea Kuwa Kitovu Cha Mafunzo na Usafirishaji wa Mafuta Kanda ya Afrika

*Waziri wa Hydrocarbons wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Mhe. Acacia Bandubola Mbongo (katikati), akiwa na Balozi wa DRC nchini Tanzania, Mhe. Jean Pierre Masala (kushoto), pamoja na Meneja wa Mipango ya Petroli wa Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA), Bw. Gilbert Jungulu (kulia), baada ya kutembelea Mfumo wa Kisasa wa Usimamizi na Ufuatiliaji wa Mafuta (SCADA) katika Ofisi za PBPA, jijini Dar es Salaam.*

Tanzania imeendelea kuimarisha nafasi yake kama kitovu muhimu cha usimamizi na usafirishaji wa mafuta katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, huku nchi jirani zikiendelea kujifunza na kutegemea miundombinu yake katika kuhakikisha upatikanaji wa nishati hiyo unaendelea kuwa wa uhakika.

Hali hiyo ilijidhihirisha kupitia ziara mbalimbali za viongozi wa Sekta ya Nishati kutoka nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na Malawi waliotembelea

miundombinu ya mafuta ya Kurasini Oil Jet (KOJ-1) iliyopo katika Bandari ya Dar es Salaam kwa lengo la kujifunza namna Tanzania inavyosimamia Sekta ya Mafuta.

Akizungumza wakati wa ziara ya kukagua miundombinu hiyo Mei 4, 2026, Waziri wa Hydrocarbons wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Mhe. Acacia Bandubola Mongo, alisema nchi yake itaendelea kujifunza kutoka Tanzania kuhusu usimamizi bora wa Sekta ya Mafuta ili kuboresha mifumo yake ya upatikanaji na usambazaji wa nishati hiyo.

Alisema DRC inategemea kwa kiasi kikubwa miundombinu ya Tanzania katika kuhakikisha kuwa upatikanaji wa mafuta unaendelea kuwa wa uhakika nchini mwake, huku ziara hiyo ikilenga kujifunza kwa vitendo namna mafuta yanavyopokelewa, kusimamiwa na kuhifadhiwa.

Aidha, Machi 24, 2026, Waziri wa Nishati na Madini wa Malawi, Mhe. Dkt. Jean Mathanga, pia alitembelea kituo hicho na kuishukuru Serikali ya Tanzania kwa mchango wake mkubwa katika kuwezesha mtiririko wa mafuta kwenda nchini Malawi.

Alisema kutokana na Malawi kutokuwa na

bandari, nchi hiyo imeendelea kutegemea kwa kiasi kikubwa miundombinu ya Tanzania katika kuhakikisha mafuta yanapatikana kwa uhakika, jambo lililosaidia kukuza shughuli za kiuchumi na kuboresha maisha ya wananchi.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Uendeshaji wa Petroli wa PBPA, Mhandisi Bruno Tarimo, alisema sehemu kubwa ya mafuta yanayoingia Malawi yanapitia Tanzania kwa kutumia Mfumo wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (BPS).

Naye Meneja Mipango ya Petroli wa PBPA, Bw. Gilbert Jungulu, alisema PBPA inasimamia kwa karibu shughuli za upakuaji na upakiaji wa mafuta kupitia mfumo wa kielektroniki wa udhibiti wa usimamizi na upatikanaji wa taarifa (SCADA).

Alieleza kuwa matumizi ya mfumo huo yanasaidia kupunguza upotevu wa mafuta kwa kiwango kikubwa na kuongeza ufanisi katika usimamizi wa mnyororo mzima wa ugavi wa mafuta nchini.

Ziara hizo zinadhihirisha namna Tanzania inavyoendelea kuwa mfano wa usimamizi bora wa Sekta ya Mafuta na kitovu muhimu cha usafirishaji wa nishati hiyo kwa nchi jirani za ukanda Mashariki, Kati na Kusini mwa Afrika.



*Waziri wa Hydrocarbons wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Mhe. Acacia Bandubola Mongo, alipotembelea miundombinu ya mafuta ya Kurasini Oil Jet (KOJ-1) iliyopo katika Bandari ya Dar es Salaam kwa lengo la kujifunza namna Tanzania inavyosimamia Sekta ya Mafuta Mei 4, 2026.*



*Waziri wa Hydrocarbons wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Mhe. Acacia Bandubola Mongo, alipotembelea miundombinu ya mafuta ya Kurasini Oil Jet (KOJ-1) iliyopo katika Bandari ya Dar es Salaam kwa lengo la kujifunza namna Tanzania inavyosimamia Sekta ya Mafuta Mei 4, 2026.*

*Waziri wa Nishati, Mhe. Deogratius John Ndejembu akizungumza wakati wa kikao chake na viongozi wa PBPA, Mamlaka ya Udhiditi wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) na kampuni ya TIPER kwa lengo la kujadili hali ya upokeaji wa mafuta yanayoingia nchini kilichofanyika Machi 26, 2026 jijini Dar es Salaam*



## **PBPA Yaagizwa Kuongeza Kasi ya Upokeaji na Usambazaji wa Mafuta Nchini**

Waziri wa Nishati, Mhe. Deogratius John Ndejembu ameutaka Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) kuhakikisha kuwa maghala yote makubwa ya usambazaji wa mafuta yanapata bidhaa hiyo kwa wakati, ili kuimarisha upatikanaji wake nchini.

Hayo yalisemwa Machi 26, 2026 jijini Dar es Salaam wakati wa kikao chake na viongozi wa PBPA, Mamlaka ya Udhiditi wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) na kampuni ya TIPER kwa lengo la kujadili hali ya upokeaji wa mafuta yanayoingia nchini.

Akizungumza katika kikao hicho, Mhe. Ndejembu amielekeza PBPA kuweka mfumo

madhubuti wa upangaji wa ratiba ya ushushaji wa mafuta (sequencing) ili kuhakikisha maghala yote makubwa yanayohusika na usambazaji yanapata mafuta stahiki na kwa wakati.

Amesema hatua hiyo itasaidia kupunguza changamoto za upatikanaji wa mafuta katika maeneo mbalimbali ya nchi.

Aidha, ameeleza kuwa Serikali imekubaliana kuharakisha ushushaji wa mafuta kwa meli zinazolingia nchini, hususan kwa ajili ya matumizi ya ndani, ili kuhakikisha upatikanaji wake unaendelea kuwa wa uhakika na salama.

Ameongeza kuwa Serikali imefanya mazungumzo na Tanzania International Petroleum Reserves Limited (TIPER), na kuelekeza kuwepo kwa utaratibu mzuri wa kupanga ushushaji wa mafuta ili wasambazaji wote wapate huduma stahiki.

Waziri Ndejembu amewaasa Watanzania kutokuwa na taharuki kuhusu upatikanaji wa mafuta, akisisitiza kuwa nchi ina akiba ya kutosha.

Vilevile, Mhe. Ndejembu, ameitaka EWURA kuhakikisha kuwa mafuta yote yanayotoka kwenye maghala yanafika kwa walengwa na kutumika ipasavyo, huku vituo vya mafuta vikihimizwa kuuza bidhaa kulingana na mahitaji halisi ya soko.

Kikao hicho pia kilihudhuriwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati anayeshughulikia Mafuta na Gesi Asilia, Dkt. James Mataragio, Mtendaji Mkuu wa PBPA, Bw. Erasto Simon, Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Dkt. James Andilile pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa TIPER, Bw. Mohamed Mohamed na wataalam wengine wa Sekta ya Mafuta



*Viongozi kutoka Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA), Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) na kampuni ya TIPER wakimsikiliza Waziri wa Nishati, Mhe. Deogratius John Ndejembu katika kikao cha kujadili hali ya upokeaji wa mafuta yanayoingia nchini kilichofanyika Machi 26, 2026 jijini Dar es Salaam*

*Waziri wa Nishati, Mhe. Deogratius J. Ndejembu (Mb.), akiwasilisha Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2026/27, tarehe 22 Aprili 2026, Bunge jijini Dodoma.*



## **NDEJEMBI: Serikali Yahakikisha Upatikanaji wa Mafuta Licha ya Vita Inayoendelea Mashariki ya Kati**

Wakati dunia ikiendelea kukumbwa na athari za vita kati ya Iran, Israel na Marekani, hofu ya kupanda kwa bei ya mafuta pamoja na upungufu wa bidhaa hiyo muhimu imeendelea kuongezeka katika mataifa mbalimbali duniani. Katika baadhi ya nchi, wananchi wameanza kushuhudia misururu mirefu kwenye vituo vya mafuta huku gharama za maisha zikiendelea kupanda kutokana na changamoto za upatikanaji wa nishati hiyo.

Hata hivyo, Serikali ya Tanzania imeendelea kuwatoa hofu wananchi kwa kusisitiza kuwa nchi itaendelea kuwa na uhakika wa mafuta licha ya changamoto zinazoendelea katika soko la dunia.

Akizungumza bungeni jijini Dodoma wakati wa uwasilishaji wa bajeti ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2026/27, Waziri wa Nishati, Mhe. Deogratius Ndejembu, alisema changamoto ya mafuta inayoendelea duniani imetokana na vita kati ya Iran, Israel na Marekani, hali iliyoathiri usafirishaji wa mafuta kupitia mlango bahari wa Strait of Hormuz, njia muhimu inayopitisha sehemu kubwa ya mafuta duniani.

“Dunia imeathirika kwa kiwango kikubwa, lakini Serikali inaendelea kuhakikisha mafuta yanapatikana nchini wakati wote,” alisema Waziri Ndejembu.

Alieleza kuwa Tanzania inaagiza mafuta kutoka nchi mbalimbali za Mashariki ya Kati zikiwemo Saudi Arabia, United Arab Emirates, Kuwait, Oman na Bahrain, huku sehemu nyingine ya mafuta ikiagizwa kupitia India.

Kwa mujibu wa Waziri huyo, uhakika wa mafuta nchini umeendelea kuimarika kupitia Mfumo wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (BPS) unaosimamiwa na Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA).

Alisema katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Tanzania ilipokea jumla ya lita bilioni 5.84 za mafuta, ambapo lita bilioni 1.63

zilikwa petroli, lita bilioni 3.94 dizeli na lita milioni 260 mafuta ya taa na ndege.

Takwimu hizo zinaonesha namna Serikali ilivyoendelea kuhakikisha upatikanaji wa mafuta hata wakati dunia ikikabiliwa na changamoto kubwa za usafirishaji wa bidhaa hiyo muhimu.

Sambamba na hatua hiyo, Serikali inaendelea na ujenzi wa matenki makubwa ya kuhifadhi mafuta eneo la Kigamboni jijini Dar es Salaam yenye uwezo wa kuhifadhi zaidi ya lita milioni 1,369. Mradi huo unatarajiwa kuongeza uwezo wa taifa kuhifadhi mafuta kwa muda mrefu zaidi na kupunguza athari zinazoweza kusababishwa na misukosuko ya soko la dunia.

Aidha, Serikali imeanza utekelezaji wa mkakati wa ujenzi wa bomba la mafuta kutoka Dar es Salaam hadi Tunduma, litakalokuwa na vituo vya kupokelea mafuta katika maeneo ya Morogoro, Makambako, Mbeya na Tunduma.

Kwa mujibu wa Waziri Ndejembu, mradi huo utasaidia kupunguza gharama za usafirishaji wa mafuta, kupunguza msongamano wa malori ya mafuta jijini Dar es Salaam pamoja na kuongeza usalama wa akiba ya mafuta nchini.

Mbunge wa Songea Mjini, Mhe. Damas Ndumbaro, aliipongeza Serikali kwa hatua mbalimbali zinazochukuliwa kuhakikisha nchi inaendelea kuwa na uhakika wa mafuta licha ya changamoto zinazoendelea duniani.

“Tanzania imeendelea kuwa na uhakika wa mafuta licha ya changamoto zinazoikumba dunia kutokana na usimamizi mzuri wa sekta hiyo,” alisema Ndumbaro alipotembelea banda la PBPA katika Maonesho ya Wiki ya Nishati yaliyofanyika kwenye viwanja vya Bunge jijini Dodoma.

Naye Mbunge wa Mbulu Vijijini, Emmanuel Nuwas, aliipongeza Serikali pamoja na PBPA kwa kuendelea kuhakikisha wananchi wanapata mafuta ya kutosha wakati wote.

Kwa upande wake, Meneja wa Sheria wa PBPA, Bi. Lilian Rwegimbura, alisema wakala huo utaendelea kuhakikisha mafuta yanapatikana kwa uhakika nchini licha ya changamoto za soko la kimataifa.

“PBPA tunafanya kazi kwa maslahi mapana ya Taifa. Uchumi wa nchi unategemea kwa kiasi kikubwa mafuta, hivyo sisi ni mhimili muhimu katika kuhakikisha shughuli za kiuchumi zinaendelea bila kukwama,” alisema Bi. Rwegimbura.

Aidha, alibainisha kuwa PBPA imeendelea kushirikiana kwa karibu na wafanyabiashara wa mafuta pamoja na taasisi za kifedha nchini ili kuhakikisha sekta ya mafuta inaendelea kukua na kuwa imara licha ya changamoto za kiuchumi zinazotokea duniani





*Afisa TEHAMA wa PBPA, Bw. George Shayo, akitoa maelezo kuhusu utendaji kazi wa flow meter zinazotumika kupokea mafuta katika Bandari ya Tanga kwa waandishi wa habari wa Gazeti la Uhuru, (hawapo pichani).*

# **Teknolojia ya SCADA Ilivyosaidia Kupunguza Upotevu wa Mafuta Nchini**

Katika miaka ya hivi karibuni, Tanzania imeendelea kuboresha Sekta ya Mafuta kwa kutumia teknolojia za kisasa zilizosaidia kuongeza uwazi, usalama na ufanisi katika shughuli za upokeaji na usambazaji wa mafuta.

Moja ya teknolojia hizo ni mfumo wa kieletroniki wa udhibiti wa usimamizi wa upatikanaji taarifa (SCADA) unaotumiwa na Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) kufuatilia kiwango cha mafuta yaliyoingia nchini kutoka melini hadi kwenye maghala ya kuhifadhi.

Mfumo huo umewekwa katika maeneo muhimu

ya upokeaji wa mafuta ikiwemo Kurasini Oil Jet, Kigamboni SBM, Bandari ya Tanga pamoja na Bandari ya Mtwara. Kupitia mfumo huo, Serikali inaweza kuona kwa wakati halisi kiwango cha mafuta kinachoingia nchini na kilichohifadhiwa kwenye maghala ya kampuni za mafuta.

Mkaguzi wa Mafuta kutoka PBPA, Bw. Issa Khamis Mwitazy, alisema mfumo wa SCADA unachangia kwa kiasi kikubwa kudhibiti upotevu wa mafuta ambao kwa muda mrefu ulikuwa changamoto katika Sekta hiyo.

Alieleza kuwa, mfumo huo hulinganisha kiwango cha mafuta kilichopokelewa kutoka melini na kiwango kilichofika kwenye maghala, endapo kutakuwa na tofauti yoyote, mfumo hutoa taarifa mara moja ili hatua zichukuliwe haraka.

“Teknolojia hii inasaidia kuongeza uwazi na kurahisisha ufuatiliaji wa mafuta kuanzia bandarini hadi kwenye maghala ya kuhifadhi,” alisema Mwitazy.

Mbali na kudhibiti upotevu wa mafuta, mfumo huo pia huongeza uwajibikaji kwa wadau wa Sekta ya Mafuta na kusaidia kuzuia uchepushaji wa mafuta kutoka eneo moja kwenda jingine bila utaratibu rasmi.

Kwa upande wake, Mtaalamu wa Mfumo wa TEHAMA kutoka PBPA, George Shayo, alisema matumizi ya mfumo wa SCADA yalipunguza kiwango cha upotevu wa mafuta kutoka wastani wa asilimia 0.5 hadi chini ya asilimia 0.1.

Alisema mfumo huo unasoma taarifa kutoka kwenye flow meters za Serikali zilizowekwa bandarini na kulinganisha taarifa hizo na mafuta yaliyomo kwenye maghala ya kampuni za mafuta.

“Faida kubwa ya matumizi ya mfumo huu ni

kwamba taarifa zote zinapatikana kwa wakati halisi. Hivyo, tofauti yoyote inapobainika inaweza kushughulikiwa haraka,” alisema Shayo.

Aidha, matumizi ya teknolojia hiyo yameongeza imani ya wadau wa ndani na nje ya nchi katika mfumo wa Tanzania wa usimamizi wa mafuta. Kutokana na mafanikio hayo, nchi kama Zambia, Malawi, Zimbabwe, Msumbiji na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo zilifika nchini kujifunza namna mfumo huo ulivyokuwa ukifanya kazi.

Msimamizi wa Uendeshaji wa Flow Meter Bandari ya Tanga, Bw. Johannes Rwezaura, alisema flowmeters zimeongeza usalama wa mafuta yanayoingia nchini. Alisema vifaa hivyo vina uwezo wa kufanya vipimo sahihi vya mafuta kabla hayajasambazwa sokoni. Pia vilikuwa na uwezo wa kuchuja uchafu ulioweza kuwepo kwenye mafuta ili kuhakikisha wananchi wanapata mafuta safi na salama kwa matumizi.

“Endapo mfumo mmoja ukipata hitilafu, kuna mfumo mwingine unaoendelea kufanya kazi bila kusimamisha operesheni. Hii inasaidia kuhakikisha huduma zinaendelea kupatikana muda wote,” alisema Rwezaura.

Naye Msimamizi wa Uendeshaji wa Flow Meter Bandari ya Mtwara, Bw. John Joseph, alisema teknolojia hiyo inasaidia kupata takwimu sahihi za mafuta yaliyoingia nchini na hivyo kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa kodi na mapato ya Serikali.

Kwa ujumla, matumizi ya teknolojia ya SCADA yanaendelea kuifanya Tanzania kuwa mfano mzuri wa matumizi ya teknolojia katika usimamizi wa Sekta ya Mafuta. Kupitia uwekezaji huo, nchi imeongeza uwazi, ufanisi na usalama katika shughuli za mafuta huku ikiendelea kuimarisha nafasi yake katika biashara ya mafuta ndani ya ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.



# Baraza la Wafanyakazi PBPA Lahimizwa Kuwa na Uadilifu Katika Kuwakilisha Maslahi ya Watumishi



*Meneja wa Fedha na Mipango wa PBPA, Bw. Kedron Mbwilo akizungumza kwa niaba ya Mtendaji Mkuu wa PBPA wakati wa ufunguzi wa Kikao cha Pili cha Baraza la Wafanyakazi kilichofanyika katika ukumbi wa Chuo cha Uongozi cha Mwalimu Nyerere, Kibaha mkoani Pwani kilichofanyika Machi 11, 2026.*

Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) wametakiwa kuzingatia uadilifu, uwazi na weledi katika kuwasilisha na kushughulikia changamoto za watumishi wanaowawakilisha, ili kuongeza ufanisi na tija katika utendaji kazi wa taasisi.

Wito huo umetolewa Machi 11, 2026 na Meneja wa Fedha na Mipango wa PBPA, Bw. Kedron Mbwilo, alipokuwa akizungumza kwa niaba ya Mtendaji Mkuu wa PBPA wakati wa ufunguzi wa Kikao cha Pili cha Baraza la Wafanyakazi kilichofanyika katika ukumbi wa Chuo cha Uongozi cha Mwalimu Nyerere, Kibaha mkoani Pwani.

Amesema Baraza la Wafanyakazi ni jukwaa muhimu linalounganisha Menejimenti na Watumishi, hivyo wajumbe wanapaswa kutekeleza majukumu yao kwa uadilifu na uwajibikaji mkubwa ili kuhakikisha masuala ya watumishi yanawasilishwa na kutatuliwa ipasavyo.


“Baraza la Wafanyakazi ni kiunganishi muhimu kati ya menejimenti na watumishi. Ni wajibu wa wajumbe kuwa waadilifu na kuwawakilisha watumishi wenzao kwa weledi mkubwa ili kuongeza tija na ufanisi katika taasisi,” amesisitiza Bw. Mbwilo.

Aidha, amewahimiza watumishi wa PBPA kuendelea kufanya kazi kwa ushirikiano na kujituma ili kuunga mkono jitihada za Serikali katika kufikia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050, ambayo kwa upande wa Sekta ya Nishati inalenga kuhakikisha Tanzania inakuwa na upatikanaji wa uhakika wa nishati ya mafuta, miundombinu imara ya mafuta pamoja na usimamizi bora wa rasilimali za petroli.

Kwa upande wake, Kaimu Meneja wa Rasilimali Watu wa PBPA, Bw. Matiko Sanawa, amewahimiza wajumbe wa Baraza hilo kutumia kikao hicho kama fursa ya kujadili kwa uwazi maoni, mapendekezo na changamoto mbalimbali zitakazochangia kuimarisha uendeshaji wa Taasisi.

*Kaimu Meneja  
Rasilimaliwatu Wakala wa  
Uagizaji Mafuta kwa Pamoja  
(PBPA), Bw. Matiko Sanawa  
akitoa neno la utangulizi  
wakati wa ufunguzi wa Kikao  
cha Pili cha Baraza la  
Wafanyakazi kilichofanyika  
katika ukumbi wa Chuo cha  
Uongozi cha Mwalimu  
Nyerere, Kibaha mkoani  
Pwani kilichofanyika Machi  
11, 2026.*





*Meneja wa Fedha na Mipango wa PBPA, Bw. Kedron Mbwilo (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya viongozi na wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi la Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) mara baada ya ufunguzi wa Kikao cha Pili cha Baraza la Wafanyakazi kilichofanyika katika ukumbi wa Chuo cha Uongozi cha Mwalimu Nyerere, Kibaha mkoani Pwani Machi 11,2026.*



*Baadhi ya viongozi na wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi la Wakala wa uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) wakifuatilia mada wakati wa ufunguzi wa Kikao cha Pili cha Baraza la Wafanyakazi kilichofanyika Machi 11,2026 katika ukumbi wa Chuo cha Uongozi cha Mwalimu Nyerere, Kibaha mkoani Pwani.*



*Daktari Johnson Katanga kutoka Taasisi ya Saratani Ocean Road (OCR) akizungumza wakati wa zoezi la utoaji elimu ya afya, upimaji wa hiari pamoja na utoaji wa chanjo dhidi ya ugonjwa wa Homa Ini lililofanyika katika ukumbi wa PBPA Jijini Dar es Salaam tarehe 30 Aprili, 2026*

# **Watumishi PBPA Wahamasishwa Kupima Afya na Kupata Chanjo ya Homa ya Ini**

Daktari Johnson Katanga kutoka Taasisi ya Saratani Ocean Road (OCR) amewahimiza watumishi wa Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) kujitokeza kupima afya zao na kupata chanjo ya kujikinga na maambukizi ya ugonjwa wa Homa ya Ini (Hepatitis B).

Wito huo umetolewa tarehe 30 Aprili, 2026 wakati wa zoezi la utoaji elimu ya afya, upimaji wa hiari pamoja na utoaji wa chanjo dhidi ya ugonjwa wa Homa Ini lililofanyika katika ukumbi wa PBPA Jijini Dar es Salaam.

Akizungumza katika zoezi hilo, Dkt. Katanga alieleza kuwa chanjo ya ugonjwa wa Homa ya Ini hutolewa kwa awamu tatu, ambapo chanjo ya kwanza hutolewa mara baada ya mhusika kupimwa na kuthibitika kuwa hana maambukizi, chanjo ya pili hutolewa baada ya mwezi mmoja, na chanjo ya tatu hutolewa miezi sita tangu kupokea chanjo ya kwanza.

Alifafanua kuwa chanjo hiyo ilianza kutolewa kwa watoto waliozaliwa mwaka 2002 ikiwa ni sehemu ya chanjo za kawaida zinazotolewa mara baada ya mtoto kuzaliwa. Kutokana na hali hiyo, watu wote waliozaliwa mwaka 2001 na kurudi nyuma wanashauriwa kupata chanjo hiyo endapo hawajawahi kuipata.

Kuhusu dalili, Dkt. Katanga alisema, mgonjwa wa homa ya ini mara nyingi haoneshi dalili zozote katika hatua za awali, hali inayosababisha watu wengi kugundua maambukizi wakiwa tayari wameathirika kwa kiwango kikubwa. Alitaja baadhi ya dalili zinazoweza kujitokeza kuwa ni pamoja na uchovu uliokithiri, maumivu ya tumbo upande wa juu kulia, macho na ngozi kuwa na rangi ya njano, kupoteza hamu ya kula, mkojo kuwa mweusi, kinyesi cheupe, pamoja na kuvimba kwa miguu au tumbo.

Aidha, alieleza kuwa maambukizi ya virusi hivyo yanaweza kutokea kupitia njia

mbalimbali ikiwemo kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto wakati wa kujifungua, kujamiiana bila kinga, kugusana na damu au majimaji ya mwili wa mtu mwenye maambukizi, kushirikiana vifaa vyenye ncha kali kama sindano, pamoja na kuongezewa damu iliyoathiriwa.

“Takwimu zinaonesha kuwa takribani watu milioni 254 duniani wanaishi na virusi vya Homa ya Ini, huku nchini Tanzania kiwango cha maambukizi kikikadiriwa kuwa asilimia 4. Hali hii inaonesha umuhimu wa kuchukua hatua mapema,” alisisitiza.

Aliongeza kuwa endapo maambukizi hayatagunduliwa mapema, kati ya asilimia 5 hadi 6 ya waathirika huingia katika hatua ya ugonjwa sugu (chronic), hali inayoweza kusababisha madhara makubwa ikiwemo saratani ya ini na hatimaye kupelekea kifo.

Kwa upande wake, Kaimu Meneja wa Rasilimaliwatu na Utawala wa PBPA, Bw. Matiko Sanawa, alisema kuwa utoaji wa elimu hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa maelekezo ya Serikali kupitia Waraka wa Utumishi Na. 2 wa mwaka 2014 unaosisitiza umuhimu wa kulinda afya za watumishi kazini. Alisema, mwajiri ana jukumu la kuhakikisha watumishi wanakuwa na afya njema ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na kuchangia maendeleo ya Taifa.

“Tumewaalika wataalamu kutoka Taasisi ya Saratani Ocean Road ili kutoa elimu, huduma ya upimaji na kutoa chanjo. Hii ni hatua muhimu katika kuhakikisha watumishi wanakuwa na afya bora,” alisema Bw. Sanawa. Huu ni Mkakati wa Serikali wa kuimarisha huduma za kinga dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza na ya kuambukiza, kwa kuhamasisha uchunguzi wa mapema na utoaji wa chanjo.





# PBPA Yahitimisha Kwa Mafanikio Ushiriki Wake Katika Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma 2026

Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) umehitimisha kwa mafanikio ushiriki wake katika Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma 2026.

Maadhimisho hayo yalifanyika katika Viwanja vya Chinangali jijini Dodoma kuanzia Juni 16 - 23 ambapo PBPA ilitoa elimu kwa wananchi na wadau kuhusu mfumo wa uagizaji mafuta kwa pamoja (Bulk Procurement System - BPS).

Akizungumza wakati wa maonesho hayo, Mkaguzi wa Mafuta wa PBPA, Issa Khamis Mwitazy, alisema maonesho hayo yamekuwa

fursa muhimu ya kuwafikia wananchi na kuwaeleza hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali kuboresha sekta ya mafuta.

"Katika kipindi chote cha maonesho tumepokea wananchi wengi waliotaka kufahamu namna mfumo wa uagizaji mafuta kwa pamoja unavyofanya kazi. Tumewaeleza jinsi mfumo huu unavyohakikisha upatikanaji wa mafuta ya kutosha nchini, kuongeza uwazi na ushindani katika ununuzi wa mafuta pamoja na matumizi ya mfumo wa kisasa wa SCADA ambao umeongeza ufanisi katika usimamizi wa mafuta na kusaidia kudhibiti upotevu wa mafuta,"

alisema Mwitazy.

Aliongeza kuwa PBPA itaendelea kutoa elimu kwa wadau ili kuongeza uelewa kuhusu mchango wa mfumo huo katika kuimarisha usalama wa nishati na maendeleo ya uchumi wa Taifa.

Katika maonesho hayo, viongozi mbalimbali waliotembelea banda la PBPA walipongeza kazi inayofanywa na Wakala huo.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Arusha, Dkt. Toba Nguvula alisema PBPA imeonyesha namna taasisi za umma zinavyopaswa kutumia maonesho kama jukwaa la kutoa elimu na kuwajengea wananchi uelewa kuhusu huduma zinazotolewa na Serikali.

"PBPA imefanya kazi nzuri ya kutoa elimu kwa wananchi kuhusu mfumo wa uagizaji mafuta kwa pamoja. Elimu hii inaongeza uelewa wa wananchi na inaonesha uwazi katika utekelezaji wa majukumu yake," alisema.

Naye Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, Ramadhan Kailima, alisema ameridhishwa na ufanisi wa mfumo wa uagizaji mafuta kwa pamoja, akieleza kuwa umeongeza uwazi, matumizi ya teknolojia na usimamizi mzuri wa sekta ya mafuta.

Kwa upande wake, Mkuu wa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW), Prof. Philipo Sanga, alisema elimu inayotolewa na PBPA ni muhimu katika kuwajengea wananchi uelewa kuhusu mchango wa sekta ya mafuta katika maendeleo ya Taifa na kupongeza juhudi za Wakala huo za kuendelea kusogeza huduma karibu na wananchi.

Kupitia ushiriki wake katika Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma 2026, PBPA imeendelea kuimarisha uhusiano wake na wananchi na wadau, huku ikithibitisha dhamira yake ya kutoa huduma kwa uwazi, ufanisi na kuendelea kuboresha mfumo wa uagizaji mafuta kwa pamoja kwa manufaa ya Watanzania wote.





# PBPA Yahamasisha Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia



*Mkurugenzi wa Uendeshaji wa Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA), Mhandisi Bruno Tarimo, akikabidhi majiko ya umeme ya matumizi madogo kwa watumishi wa PBPA kufuatia kampeni ya kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia, iliyolenga kuongeza uelewa na matumizi ya teknolojia hiyo miongoni mwa watumishi.*

Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) umechukua hatua madhubuti ya kuhamasisha matumizi ya Nishati Safi kwa kuwagawia watumishi wake majiko ya umeme, ikiwa ni sehemu ya juhudi za makusudi za kuhamasisha mabadiliko ya matumizi ya nishati nchini.

Akizungumza katika tukio hilo, Mkurugenzi wa

Uendeshaaji wa PBPA, Mhandisi Bruno Tarimo, amesema hatua hiyo inalenga kuimarisha juhudi za taasisi katika kuhamasisha jamii kuhusu matumizi ya nishati safi na salama kwa matumizi ya kila siku.

Ameeleza kuwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia sera mbalimbali za kitaifa na kimataifa, imeendelea kutambua umuhimu wa nishati safi ya kupikia kama nyenzo muhimu ya kukabiliana na changamoto za kimazingira, kiafya, kijamii na kiuchumi.

“PBPA inatekeleza jukumu muhimu katika kusaidia juhudi za Serikali za kuhakikisha asilimia 80 ya Watanzania wanatumia nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2034. Ugawaji wa majiko janja aina ya pressure cooker kwa watumishi ni sehemu ya mkakati huo,” amesema Tarimo.

Aidha, amewataka wanufaika wa majiko hayo kuyatumia ipasavyo na kuwa mabalozi wa kuhamasisha matumizi ya nishati safi katika jamii zao ili kuongeza uelewa na kuharakisha mabadiliko ya matumizi ya nishati nchini.

Kwa upande wake, Afisa Dawati wa Nishati Safi ya Kupikia kutoka PBPA, Bi. Hilda Kowero, amesema kuwa Serikali imeweka mkakati maalum wa nishati safi ya kupikia unaolenga kuboresha maisha ya wananchi kupitia matumizi ya teknolojia rafiki kwa mazingira.

Amefafanua kuwa matumizi ya majiko ya umeme husaidia kupunguza utegemezi wa kuni na mkaa, hivyo kulinda misitu, kupunguza ukataji wa miti na kuboresha afya kwa kupunguza madhara ya moshi yanayosababisha magonjwa ya njia ya hewa.

Katika kuhakikisha matumizi sahihi na salama ya majiko hayo, watumishi walipatiwa mafunzo maalum kuhusu namna bora ya kuyatumia, kutunza na kuzingatia tahadhari za usalama. Mafunzo hayo yalijumuisha matumizi sahihi ya umeme, njia za kupunguza matumizi ya nishati, pamoja na mbinu za kupika kwa ufanisi kwa kutumia majiko ya shinikizo (pressure cooker). Hatua hiyo inalenga kuwajengea watumishi uelewa wa kina ili waweze kunufaika kikamilifu na teknolojia hiyo na kueneza maarifa hayo kwa jamii inayowazunguka.

Bi. Kowero ameongeza kuwa PBPA itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kuhamasisha mabadiliko ya tabia kwa wananchi ili kuongeza matumizi ya nishati safi na kuchangia katika ujenzi wa jamii yenye afya bora na mazingira endelevu.





**Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA)**  
**Sanduku la Posta 2634,**  
**Dar es Salaam, Tanzania,**  
**[info@pbpa.go.tz](mailto:info@pbpa.go.tz).**  
**+255 222 129 009**



**PbpaTanzania**



**PbpaTanzania**



**[pbpa\\_tanzania](#)**